

Public education  
Discover a world of opportunities

## KUANDIKA NA KUSEMA HERUFI KUSOMEA NYUMBANI

### KUANDIKA NA KUSEMA HERUFI NI MHIMU!

Kuzungumza na kusikiliza ndio misingi ambayo maandishi, herufi na kusoma hujengwa. Mtoto wako huendelea haya na ujuzi mwingine wakati wanahudhuria Chekechea. Wakati wanajenga maneno yao na kusikiliza kwa kujiamini, wanaanza kujifunza kuhusu uandishi.

#### Ninaweza kufanya nini?

- Soma na mtoto wako mara kwa mara. Chunguza maneno na vitabu pamoja na kuwashirikisha wakati unaandika.
- Unaposoma pamoja, zungumzia juu ya maneno unayoyasoma. Kwa mfano, sauti ya maneno kama: bat na cat, na zungumzia sauti zilizofanywa mwanzoni mwa maneno. Wakati mtoto wako ana starehe, jadiliana juu ya sauti zilizotengenezwa mwishoni mwa maneno.
- Himiza mtoto wako kukusaidia kuandika maelezo, barua pepe na orodha ya ununuzi Andaa karatasi na penseli ili waweze kujaribu kuandika na wewe.
- Cheza michezo ya maneno kwa pamoja kama vile kutafuta maneno.

**Mtoto mlemavu kwa kawaida anafaidika na kufurahia kutokana na mwingiliano wa karibu na kulisimua unaotolewa wanapokuwa wakisoma hadithi zao wanazozipenda au nyimbo zinazoimbwa za kitalu. Kama mtoto wako ana ulemavu, shule zao zinasaidia wao kushiriki katika shughuli katika ngazi zinazofaa kwa uwezo wao. zungumza na mwalimu wa mtoto wako kuhusu zana sahihi, vifaa na mawazo ya kusaidia wewe na mtoto wako.**

**Kama mtoto wako anazungumza lugha nyingine au lahaja, wanahitaji muda wa kusikia sauti ya lugha ya Kiingereza. Inaweza kuchukua hadi miaka miwili au zaidi kwa wao kusikia na kusema sauti hizi zote.**

- Bandika barua na michoro ya mtoto wako aliyounda. Viandikie maelezo kama vile: *Mimi ninajivunia sana kwa wewe!*
- tumia sumaku kubandika maneno ya herufi juu ya friji au ubao wa sumaku. Saidia mtoto wako kutengeneza maneno.
- Tafuta maneno nyumbani, wakati wewe uko mahali popote, wakati ukiwa unatembea na wakati wewe unasafiri kama vile juu ya ishara na katika maduka.
- Weka ubao wa ujumbe nyumbani na kuandika jumbe kwa ajiri ya mtoto wako. Watie moyo kukuachia jumbe wewe na ndugu za familia wengine.
- Fanya matumizi mazuri ya barua zisizo muhimu! Uliza mtoto wako:
  - Zungushia mduara kwa maneno fulani kama vile *m* na sauti fulani kama vile *sh*
  - piga mstari maneno yote mawili, maneno matatu na kadhalika
  - Hesabu ni mara ngapi wanaweza kupata neno fulani kama *vile* - hii inawasaidia kutambua maneno ya kawaida.

**Zima televisheni. Ni rahisi kwa mtoto wako kuwa makini wakati hakuna usumbufu.**



Department of  
Education

**Utakuta masomo zaidi kwenye  
Vifurushi vya habari za nyumbani  
kwenye [education.wa.edu.au](http://education.wa.edu.au).**